



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Kama inavyofahamika, Zoezi la Kuandikisha Wapiga Kura katika mfumo mpya wa kielektroniki (BVR) ulianza Februari, 23, 2015 mkoani Njombe. Zoezi lilianza na mashine 250 tu. Baada ya Njombe, vifaa yaani mashine zilianza kupokelewa kwa awamu jinsi Zoezi lilivyoendelea mikoa kwa mikoa hadi kufikia jumla ya mashine 8,000 kwa nchi nzima. Ni mashine hizi ndizo zimekuwa zikihamishwa mikoa mbalimbali hadi Mkoa wa Dar es Salaam ambapo Zoezi linaendelea hadi sasa.

Kwa vile Dar es Salaam ina idadi kubwa ya watu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliona ni mwafaka Zoezi hili lifanyike mwisho. Wakati Zoezi likiendelea Dar es Salaam, uandikishaji pia ulifanyika na kukamilika Zanzibar kwa muda wa siku tatu (3). Hii ni kwa sababu watu wengi Zanzibar tayari wameandikishwa katika Daftari la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Kwa upande wa Zanzibar Tume (NEC) hutumia pia Daftari la (ZEC).

Kwa kuwa Ratiba ya NEC inakwenda hadi tarehe 25 Oktoba, 2015, siku ya Uchaguzi, na kwa uchache wa mashine, nchi nzima Tume iliweka Ratiba ya kukamilisha Zoezi Mkoa kwa Mkoa ili Daftari liwe tayari inapofika wakati wa Uteuzi wa Wagombea. Hivi ndivyo ilifanyika katika Mikoa yote. Hivyo, siku zilizopangwa kumaliza Zoezi la Uandikishaji Mikoani zilipotimia, Tume iliweza kuongeza muda ili kumaliza kuandikisha Wananchi waliojitokeza vituoni siku hiyo. Kwa ujumla, nchi nzima hadi jana tarehe 29 Julai, 2015, Takwimu zinaonesha jumla ya Wananchi

18,826,718 wamejiandikisha wakati Zoezi bado linaendelea Dar es Salaam.

Kwa mantiki hiyo, kwa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kuzingatia mwamko mkubwa ulioonekana Wananchi kujitokeza kwa wingi isivyo kawaida katika Vituo mbalimbali, Tume imeamua kuongeza muda wa kumalizia watu watakaokuwa wapo vituoni siku ya mwisho yaani kesho tarehe 31 Julai, 2015. Sasa muda umeongezwa kwa siku nne

**KUMALIZIA UANDIKISHAJI HUO.**

Tume inawashukuru Wananchi wa Dar es Salaam kwa kuwa wavumilivu wakati wa Zoezi hilo na waendeleo kushirikiana ili kufanikisha Zoezi hili ambalo limeanzishwa kwa nia njema ili kila mwenye sifa aliyejiandikisha aweze kutumia haki yake ya kikatiba kuchagua Viongozi wanaowataka.

ASANTENI,

Jaji (Mst.) Damian Z. Lubuva  
**MWENYEKITI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**